# مِنْ خُرَافَاتِ دِيْنِ الشّيْعَةِ الإثْنَيْ عَشَرِيّةِ

## (مُوْجِبَاتُ الفَقْرِ)

# MIONGONI MWA UZUSHI WA DINI YA SHIA ITHNAASHARIYYA

## (MAMBO YENYE KUPELEKEA UFAKIRI/UMASKINI)

**Imeandaliwa na:**

**Abu Halima Arafat**

بسم الله الرحمن الرحيم

Hakika kila sifa njema anastahiki Allaah Subhaanahu Wata'alaa na Swala na Salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad, Jamaa zake na Maswahaba wote.

Ndugu msomaji, hii ni Makala fupi katika mfululizo wa kubainisha uhalisia wa kundi la Shia Ithnaashariyya katika kuweka wazi Itikadi zao lakini pia kubainisha baadhi ya mambo ya Uzushi na Vituko mbalimbali vilivyomo ndani ya vitabu vyao, tunafanya hivyo ili kuwafahamisha watu ubatili wa pote hilo, pia kujua kwamba ni pote ambalo liko mbali na mafunzo sahihi ya Mtume swala na salamu zimshukie na Maswahaba wake.

Ndugu msomaji, utashuhudia mambo mengi ya ajabu ndani ya Makala hii ambayo inatosheleza kwa mtu mwenye akili timamu na mwenye uwezo wa kutafakari mambo kuelewa tafauti iliyopo baina ya Uislamu na Dini ya Shia.

Kutokana na wingi wa mambo yao ya Uzushi na hapa si mahali pa kutaja mengi katika hayo nimechagua baadhi yake kama sehemu ya mfano, kama tulivyofanya kwenye ile risala yetu **(Ni Nani Shia Ithnaashariyya?)** ambayo nimetaja ndani baadhi ya Uzushi na Uwongo wao na hapa nitaitaja mifano miwili:

1. **"Hakuna kwenye Mikojo wala Mavi ya Maimamu (12) kitu chenye kuchukiza, si harufu wala uchafu, bali ni sawa na Miski kali. Mwenye kunywa Mikojo, Mavi na Damu yao Allaah hatomuingiza motoni na ni wajibu wake kumuingiza peponi!!"**[1].
2. **"Kuvaa viatu vyeusi kunarefusha dhakari na kudumisha huzuni**[2]**, na kuvaa viatu vya njano kunaitia nguvu dhakari na kuondosha huzuni"**[3].

Makala yangu hii nimeiita: **"Miongoni mwa Uzushi wa Dini ya Shia Ithnaashariyya)**.

Namuomba Allaah aniruzuku Ikhlaas katika kauli na matendo na atuongoze sote katika njia yake iliyonyooka. Walaahu A'alam.

---

[1]- Kitabu: [Anwaarul Wilaaya] (Uk. 440) cha mwanachuoni wao Alkalbaakani.
[2]- Kitabu: [Usuulul Kaafi] (Jz. 6, Uk. 465) cha mwanachuoni wao Al-Kulain.
[3]- Kitabu: [Al-Furuu'minal Kaafi] (Jz. 6, Uk. 465) cha mwanachuoni wao Al-Kulain.

قال شيخهم عبد الله الْمَامَقَانِيُّ في كتابه: [مِرْآةِ الْكَمَالِ] (ج٢، ص٥٦٩-٥٨٢) :

"أَنَّهُ قَدْ وَرَدَ كَوْنُ أَشْيَاءَ مِنَ الْمَكْرُوْهَاتِ وَالْمُحَرَّمَاتِ مُوْجِبَاتٍ لِلْفَقْرِ"

**Amesema sheikh wao Abdullaah Al-Maamaqaani: "Imekuja kwamba kuna miongoni mwa mambo ya karaha na haramu (mambo) yenye kupelekea kwenye ufakiri/umaskini"[4].**

Miongoni mwa mambo yenye kusababisha ufakiri na umaskini) ni:

مِنْهَا: كَثْرَةُ النَّوْمِ عُرْيَانًا.

1. **"Kukithirisha kulala Uchi (bila ya nguo".**

تَرْكُ غَسْلِ الْيَدَيْنِ عِنْدَ الْأَكْلِ.

2. **"Kuacha kuosha mikono miwili wakati wa (kuanza) kula.**

الْقُعُوْدُ عَلَى أَسْكُفَةِ الْبَيْتِ، وَهِيَ الْعَتَبَةُ الَّتِيْ تُوْطَأُ عَلَيْهَا.

3. **"Kukaa katika kizingiti cha mlango", nayo ni sehemu ambayo watu hukanyaga (kwa ajili ya kuingia au kutoka ndani).**

كَنَسُ الْبَيْتِ فِيْ اللَّيْلِ وَبِالثَّوْبِ وَالْخِرْقَةِ.

4. **"Kufagia nyumba wakati wa usiku kwa kutumia nguo au kitanbara".**

غَسْلُ الْأَعْضَاءِ فِيْ مَوْضِعِ الِاسْتِنْجَاءِ وَالْوُضُوْءِ هُنَاكَ.

5. **"Kuoga au kutia udhu mahali pa kustanji (chooni, sehemu inayotumika kwa kukidhi haja ndogo au kubwa".**

مَسْحُ الْوَجْهِ أَوْ مُطْلَقِ الْأَعْضَاءِ الْمَغْسُوْلَةِ بِالذَّيْلِ وَالْكُمِّ.

6. **"Kupangusa uso au kiungo kingine chochote kilichooshwa kwa kutumia ncha au mkono wa nguo".**

وَضْعُ الْقِصَاعِ وَالْأَوَانِيْ غَيْرَ مَغْسُوْلَةٍ.

7. **"Kuacha sahani na vyombo vingine bila kuviosha".**

---

[4]- Kitabu: [Mir-aatul kamaal] (Jz. 2, Uk. 569-582):

قَلْمُ الْأَظْفَارِيَوْمَ الْأَحَدِ، فَإِنَّهُ يَذْهِبُ بِالْبَرَكَةِ.

8. **"Kukata kucha siku ya jumapili, kwa sababu kunaondoa baraka".**

الأَكْلُ عَلَى ظَهْرِ الْجَمَلِ.

9. **"Kula ukiwa upo juu ya mgongo wa ngamia".**

إِلْقَاءُ النُّخَامَةِ وَالرِّيْقِ عَلَى الْخَلَاءِ.

10. **"Kutema kohozi au mate chooni".**

البَوْلُ فِي الْمَاءِ.

11. **"Kukojoa katika maji".**

النَّوْمُ عَلَى غَيْرِوُضُوْءٍ.

12. **"Kulala bila ya kutia Udhu".**

النَّوْمُ فِي الْعَصْرِ.

13. **"Kulala wakati wa alasiri".**

التَّصْفِيْقُ بِالْيَدِ.

14. **"Kupiga makofi kwa mikono".**

أَكْلُ الْفُوْمِ وَالْبَصَلِ غَيْرَ الْمَطْبُوْخَيْنِ لَيْلَةَ الْجُمُعَةِ.

15. **"Kula kitunguu thoumu na kitunguu maji kabla ya kupikwa usiku wa ijumaa".**

شُرْبُ الْمَاءِ مِنَ الْكُوْزِ الْمَكْسُوْرِ، وَكَذَا الْأَكْلُ مِنَ الْآنِيَةِ الْمَكْسُوْرَةِ.

16. **"Kunywa maji katika kikombe kilichovunjika, kadhaalika kula katika chombo kilichovunjika".**

الِاخْتِلَاطُ مَعَ الْأَزْرَقِ وَأَصْفَرِ اللِّحْيَةِ.

17. **"Kuchanganyika ndevu za rangi ya bluu na njano".**

وَضْعُ الْيَدِ تَحْتَ الذَّقْنِ.

18. **"Kuweka mkono chini ya kidevu"**

الجِمَاعُ فِي الْمَاءِ الْحَارِّ.

**19. "Kufanya jimai (ndani ya maji ya moto".**

تَعْجِيْلُ الْخُرُوْجِ مِنَ الْمَسْجِدِ.

**20. "Kuharakisha kutoka msikitini".**

تَعْجِيْلُ الْبُكُوْرِ إِلَى السُّوْقِ.

**21. "Kurauka mapema kwenda sokoni".**

تَأْخِيْرُ الرُّجُوْعِ عَنِ السُّوْقِ.

**22. "Kuchelewa kurudi sokoni".**

خِيَاطَةُ الثَّوْبِ عَلَى الْبَدَنِ.

**23. "Kushona nguo ikiwa mwilini".**

إِطْفَاءُ السِّرَاجِ بِالنَّفْخِ وَالنَّفْثِ.

**24. "Kuzima taa kwa kupuliza na kuvivia".**

قَصُّ الْأَظْفَارِ بِالْأَسْنَانِ.

**25. "Kukata kucha kwa kutumia meno".**

لَبْثُ الْجُنُبِ فِي الْمَسْجِدِ.

**26. "Kukaa mwenye janaba msikitini".**

إِلْقَاءُ الْقُمَّلِ قَبْلَ قَتْلِهَا.

**27."Kumtupa chawa kabla ya kumuuwa".**

قَتْلُ الْقُمَّلِ فِي الْمَسْجِدِ

**28. "Kumuuwa chawa ndani ya msikiti".**

الذَّهَابُ إِلَى الْخَلَاءِ حَافِيًا وَمَكْشُوْفَ الرَّأْسِ

**29. "Kwenda chooni miguu chini (bila viatu) na hali ya kuwa kichwa wazi".**

النَّظَرُ إِلَى تَارِكِ الصَّلَاةِ.

**30. "Kumtazama mtu mwenye kuacha swala (mtu asiyeswali)".**

النَّظَرُ إِلَى الْمِرْآةِ بِاللَّيْلِ.

**31. "Kutazama kioo wakati wa usiku".**

Bali wanadai kuna mambo yanapelekea kwenye uchizi au wazimu:

أَكْلُ التُّفَّاحِ الحَامِضِ.

**32. "Kula tufaha (Apple) ng'wadu/chachu".**

قِرَاءَةُ أَلْوَاحِ الْقُبُوْرِ

**33. "Kusoma mbao za makaburini".**

Na hapa nitataja ziada ya vituko, uwongo na uzushi wao, mfano:

- Shia Ithnaashariyya wanasema**: "Udongo wa kaburi la Hussein ni tiba ya kila maradhi"(5).**
- Shia Ithnaashariyya wanasema: **"Mtoto anaezaliwa kwa ndoa ya Muta' (ndoa ya muda) ni bora zaidi kuliko wa ndoa ya kudumu"(6).**
- Shia Ithnaashariyya wanasema: **"Watu wote ni watoto wa zinaa isipokuwa Shia"(7).**
- Shia Ithnaashariyya wanasema: **"Kutazama Uchi wa asiyekuwa muislamu ni sawa na kutazama kwako Uchi wa punda!!"(8).**

**Na Swala na Salamu zimshukie Mtume wetu Muhammad.**

**Abu Halima Arafat.**
**Jumanne: 1/dhulqa'dah/1443H – 31/05/2022M**
**Pongwe Tanga**
**Tanzania.**
**Simu: +255 715 263 253**

5- Kitabu: [Al-Mazaar] (Uk. 125). Cha mwanchuoni wao Al-Mufid.
6- Kitabu: [Al-Istibswaar] (Jz. 3, Uk. 155). Cha mwanachuoni wao Abu Ja'far At-Tuusi.
7- Kitabu: [Ar-Raudhu minal Kaafi] (Jz. 8, Uk. 285). Cha mwanachuoni wao Al-Kalain.
8- Kitabu: [A-Furuu' minal Kaafi] (Jz. 6, Uk. 501). Cha mwanachuoni wao Al-Kulain.